

LEARNING BY EAR

“The Lost Kid – the Story of Single Mothers in Africa”

EPISODE 9: “Cutting one's own hand”

AUTHOR: Mantegaftot Sileshi Siyoum

EDITOR: Stefanie Duckstein, Adrian Kriesch

PROOFREADER: Kate Hairsine

List of characters by scene:

SCENE ONE: NIGHT AT MR. KASU COMPOUND

- Chala (m, 17)
- Mekete (m, 16)
- Jonas (m, 15)
- Mr. Kasu (m, 60)
- Narrator (m, around 35)

SCENE TWO: NIGHT AT PAPA TILAHUN'S HOUSE

- Aster (f, 15)
- Narrator (m, around 35)

SCENE THREE: NIGHT AT KASSECH'S ROOM

- Kassech (f, 22)
- Begidu (m, 7)
- Narrator (m, around 35)

SCENE FOUR: NIGHT OUTSIDE MR. KASU’S COMPOUND

- **Chala (m, 17)**
- **Mekete (m, 16)**
- **Police (m, 32)**
- **Narrator (m, around 35)**

INTRO:

Hamjambo, wapendwa wasikilizaji, na karibuni kwenye mchezo wetu wa redio wa Noa Bongo Jenga Maisha Yako uitwao “MWANA MPOTEVU- KISA CHA KINA MAMA WANAOWALEA WATOTO WAO BILA BABA ZAO BARANI AFRIKA”. Kisa hiki kinawatia shime kina mama wa watoto wasio na waume washughulikie vyema malezi ya watoto wao tangu wakiwa wachanga. Kama mjuavyo, watoto ndio mhimili wa maisha yetu ya siku za usoni. Kwa hivyo, tunapaswa kuwashughulikia ipasavyo kila kukicha. Sehemu ya leo ni ya tisa na inaitwa “MSIBA WA KUJITAKIA”. Sehemu hii inaanzia pale tulipoachia kwenye sehemu ya nane. Katika sehemu hiyo, Jonas na marafiki zake wawili walikuwa wamepanga kuvamia nyumba ya Bwana Kasu. Mbwa wa Bwana Kasu hakusita kubweka kwa hivyo wavulana hao watatu wakaamua kupitia upande wa nyuma kutafuta njia ya kuingilia nyumba ya bwana huyo tajiri. Kutokea upande wa nyuma wa nyumba tunawapata vijana hao wakizozana kwa sauti ya chini.

SCENE ONE: NIGHT AT MR. KASU’S COMPOUND

1. SFX: DOG BARKING

2. SFX: WIND BLOWS, NIGHT AMBIANCE

3. Mekete: (whispers throughout the conversation)

Shida yote hii ni kwa sababu yako, Challa! Lau tungekuwa na kipande cha nyama chenye sumu, tungekuwa tumeshamkomesha kitambo huyo mbwa fedhuli.

- 4. Challa:** Sikujua kwamba huyo mbwa wangu mpumbavu angekifukua hicho kipande cha nyama.
- 5. Jonas:** Natumai hajala nyama hiyo.
- 6. Challa:** Hayanihusu hata kidogo! Ninamchukia.
- 7. SFX: DOG BARKING STOP**
- 8. Jonas:** Sshhh, sikizeni! Mbwa ameacha kubweka.
- 9. Challa:** **(In a hurry)** Haya! Tuuparamie ukuta! Nipeni kamba.
- 10. Mekete:** Subiri, subiri! Ebu kwanza nichungulie nione yanayoendelea huko ndani.
- 11. Challa:** Kote kuna giza.
- 12. Mekete:** Bila shaka huyo bwana sasa hivi amelala fofofo **(laughs)**.
- 13. Jonas:** Challa, una hakika kwamba Bwana Kasu yuko peke yake nyumbani?
- 14. Challa:** Naam! Mchana nilipokuja kufukia kile kipande cha nyama, nilimuona mwanamke mmoja na

wasichana watatu wakiondoka kwa gari.
Nadhani walikuwa wakienda likizoni.

15. Jonas: Naam, Nilichunguza mambo ya hii familia siku chache zilizopita- huyo mwanamke ni mke wa huyu bwana, na hao wasichana watatu ni mabinti zake. Kitendawili kimeshaaguliwa!
(Laughs)

16. Mekete: Kwa hivyo amewapeleka likizo mkewe na mabinti zake ili abaki akijikoromea pekee katika jumba hili kubwa **(All laugh in a low voice)**.

17. Challa: Vyovyote vile! Tulivamie hilo jumba sasa hivi!

18. Jonas: Sawa! Nitatangulia, nisaidieni kupanda ukuta.

19. Mekete: Sawa, Jonas.

20. Challa: Sasa, panda kwenye mabega yetu.

21. Jonas: Sawa! subiri... **(they hold him up)** Sasa, ninaweza kuruka. **(He jumps in the compound)**.

22. SFX: SOMEONE LANDS ON THE GROUND

23. SFX: DOG BARKS AT THE FRONT COMPOUND

24. Jonas: (Whisper) Haya, jamaa njooni, fanyeni chapuchapu!

25. SFX: THE HOUSE DOOR OPENS SUDDENLY

26. SFX: GUN IS BEING CHARGED

27. Mr Kasu: (Loud) Usisogee hatua moja! Wewe nani? Mikono juu!

28. Mekete: Balaa! Tuondoke hapa! Mbio!

29. Challa: Harakisha!

30. SFX: DOG STILL BARKING

31. SFX: SOMEONE RUNS

32. Mr Kasu: Simama hapo ulipo ama nitakupiga risasi.
(running continues)
Nimesema, SIMAMA!

33. SFX: GUN SHOTS

34. Mekete: (Very shocked) Mungu wangu! Amempiga risasi!

35. Challa: Balaa, balaa, balaa! Tuonoke hapa haraka!

36. Mr Kasu: Simameni! Nyinyi wawili hapo, msimame mara moja au nitawapiga risasi!

37. SFX: GUN SHOTS, TWICE

38. Mekete and Challa: (scream while the gun shoots).

39. SFX: TWO PEOPLE JUMPING ON THE GROUND

40. SFX: THE WIND BLOWS STRONGLY

41. SOMEONE WALKING SLOWLY

42. Mr. Kasu (Shocked) Nini!? Jonas! Mwanangu, (sobs) Nimejisababishia msiba, nimejitakia msiba! (More sobs, and after a while he cries out aloud) Laaaaaaa!

43. NARRATOR: Tukio la kusikitisha! Bwana Kasu amempiga mwanawe risasi. Bwana Kasu aliwatelekeza kabisa wanawe Kassech na Jonas tangu alipoachana na mama yao miaka mingi iliyopita. Wenyewe watoto hawakuwa na habari kwamba baba yao ni huyo Bwana Kasu. Majuto sasa hayafai. Kasu hakudhani kama angekumbwa na jambo la kumkumbusha maisha yake ya zamani lakini kadari imemjaalia kukutana na mwanawe kwa njia isiyoelekea. Kweli amemuua mwanawe? Na vipi marafiki zake Jonas? Endelea kututegea sikio. Wakati huo huo, msichana mchanga, Aster anaandika barua yake ya kwanza ya mapenzi.

SCENE TWO: NIGHT AT PAPA TILAHUN HOUSE

44. SFX: NIGHT AMB FROM OUTSIDE, PAPER BEING RIPPED

45. Aster: **(Monologue)** Yarabi, nina nini mimi?
Ninaandika nini mimi? Kweli nina hisia za
mapenzi? Hapana! **(She crumples the paper
and throws it in a trash).**

46. SFX: PAPER BEING CRUMPLED

47. SFX: PAPER BEING THROWN IN A WASTEPAPER

48. Aster: La! Lazima nimwandikie barua! Nimechoka
kuteseka! Haya! Nitaanza vipi? **(Pause)**
Mpendwa Jonas... Ninakupenda sana!
Hapana! Sivyo! Sawa... **(inhales and exhales
deeply).**

KW begin

49.SFX: WRITING FIRMLY ON A PAPER

50.Aster: Kila mara, ninapokufikiria, ninaumia moyoni,
nasikia mwili wangu ukiwaka na kutetemeka
kwa huba zako. Huhisi kama kwamba kichwa
kitaripuka! **(she breathes deeply in a stress)**

Naam! **(Pause)** Hapana! Maneno hayawezi
kuelezea hisia vizuri.

51. SFX: PAPER BEING TORN

KW end

52. SFX: CELL PHONE DIALING

53.Aster: **(Talking on the cell phone)** Halo! Semira,
mwanadani... Hapana, Begidu na Kassech
wako salama... Naam, hawana neno! Pengine
wamelala **(Sobs)** ... La, hakuna kitu! Usemayo
ni kweli Semira, nina hisia za mapenzi! **(More
sobs)**... Hapana, nitakwenda sasa hivi
nikamweleze! ... Kweli, usemayo ni kweli, sijui
hata yuko wapi ... Sawa, Semira, nitafanya
hivyo kesho asubuhi... Asante sana, rafiki
yangu! ...Haya...kwaheri!

54. SFX: HANGING UP CELL PHONE

55. Aster: **(More sobs)**

56. NARRATOR: Aster anashindwa kujizuia machozi yanayomtoka
njia mbilimbili. Ndiyo mara yake ya kwanza kuhisi kumpenda mtu jinsi
hiyo. Tutoke kwa Aster twende chumbani kwa Kassech. Kassech
yumo katika harakati ya kujibu maswali yote anayoulizwa na

mwanawe jasiri, Begidu. Tangu Begidu aliporejea nyumbani baada ya kutoweka kwa muda, Kassech amekuwa akijitahidi kumpa malezi mema.

SCENE THREE: NIGHT AT KASSECH'S ROOM

57. SFX: NIGHT AMBIENCES

58. **Kassech:** Moto wa mkaa umezimika na kuna baridi nje.
Acha nifunge mlango.

59. **Begidu:** Naam, mama, kuna baridi!

60. SFX: DOOR BEING CLOSED

61. SFX: CORN IS BEING BOILED

62. **Begidu:** Ma?

63. **Kassech:** Naam, Begidu mwanangu?

64. **Begidu:** Utanipa mahindi yakishaiva?

65. **Kassech:** **(Joyfully)** Bila shaka! Ni yako, mwanangu.

66. **Begidu:** Unanipenda, ma?

67. **Kassech:** Tena sana, mwanangu! **(She kisses him on**

his cheek repeatedly).

68. **Begidu:** Hutanipiga tena?

69. **Kassech:** Begidu, mwanangu. SITAWAHI TENA!

70. **Begidu:** Ninakupenda, mama.

71. **Kassech:** Na mimi pia ninakupenda kwa dhati,
mwanangu!

72. **Begidu:** Mahindi yataiva lini?

73. **Kassech:** Hivi punde! Ebu nipindue mkaa kwenye jiko.

74. SFX: STOVE BEING SHAKEN

75. **Begidu:** Niupepee moto?

76. **Kassech:** Naam, tumia hilo pepeo la minyaa.

77.SFX: FANNING THE CHARCOAL

KW BEGIN

78. **Begidu:** **(Fans the charcoal)** Mama, utaacha lini?

79. **Kassech:** Kwa nini, Begidu?

80. **Begidu:** Baadhi yao hunikejeli mara nyingine.
81. **Kassech:** Niambie, kwani huwa wakisema nini?
82. **Begidu:** Mara nyingine wao huniita “mtoto wa mkaa”.
83. **Kassech:** Usiwajali hao watoto mwanangu. Kila kazi ni muhimu! **(thoughtful)** Ingawa ninapouza mkaa, ninaishia kuharibu mazingira.
84. **Begidu:** Mbona, mama?
85. **Kassech:** **(Patiently)** Kwa sababu mkaa unatokana na miti. Tunapokata miti kwa kasi, tunaishia kukosa misitu.
86. **Begidu:** Ninafahamu.
87. **Kassech:** Haya! Tazama, tunachemsha mahindi yetu kwa kutumia moto wa mkaa.
88. **Begidu:** Ndiyo.
89. **Kassech:** Watu hukata miti mingi na kuharibu misitu ili wachome makaa. Hii ndiyo sababu misitu yetu inaendelea kutoweka. Wakati mwingine shirika kubwa la kilimo hufyeka sehemu kubwa ya m situ, ikiwemo miti ya zamani sana, kwa kutumia matingatinga makubwa, ili kupanda mimea ya

mazao. Hii ni sababu nyingine ya misitu
kuendelea kutoweka.

90. Begidu: Aha, lakini pia si vibaya kwa sababu tunaweza
kuchemsha mahindi yetu.

91. Kassech: **(Laughs)** Wewe ni mtoto mwerevu sana!
Naam, makaa ni muhimu sana lakini pia si
vizuri kuharibu misitu

92. Begidu: Una maana kwamba mkaa ni mzuri.

93. Kassech: Nina maana kwamba, mkaa na vitu kama vile
kuni ni muhimu maishani mwetu.

94. Begidu: Mbona usinunue kitu kingine tofauti na mkaa?

95. Kassech: Sasa hivi, ninatumia mkaa kwa sababu siwezi
kugharamia nishati ya umeme. Nishati ya
umeme inahitaji hela. Mimi hapa nilipo ni
mwanamke maskini.

96. Begidu: Wewe si maskini, ma.

97. Kassech: Ukizingatia masomo yako, basi sitakuwa
maskini tena.

98. Begidu: Naam! Nitayazingatia. Lakini mama, utaacha
lini kutumia mkaa?

99. Kassech: Wakati nitakapopata fedha za ziada. Ninafanya kazi kwa bidii, lakini hivi karibuni nataka pia kurudi kwenye masomo ya jioni. Ukijitahidi shuleni bila shaka utapata vitu vyote unavyotamani.

100. Begidu: Basi, nitajitahidi nifanye vyema shuleni. Nikiwa mkubwa, nitakuwa mwanasayansi kisha nivumbue kitu kingine cha kupikia badala ya mkaa na hapo hutauza tena mkaa.

KW End

101. Kassech: Mtoto wangu mzuri! **(Kisses him on the cheek)**. Mahindi tayari.

102.SFX: COOKING POT'S LID BEING LIFTED

103.SFX: BOILING

104. NARRATOR: Kassech anatambua jinsi mwanawe anavyojawa na furaha pale anapomshughulikia zaidi. Shirika la Umoja wa Mataifa la Kushughulikia Watoto, ama UNICEF ndilo linaloshughulikia maslahi ya watoto. Shirika hilo lina hati inayoelezea kwamba watoto wanahitaji kuwasiliana vyema na wazazi, jamaa au walezi wao. Hati hiyo inasema pia kwamba watoto wote wana haki sawa, kila mtoto anapaswa kutunzwa kiafya, na kila mtoto ana haki ya masomo. Hasa watoto wachanga wasiozidi umri wa miaka sita wanahitaji uangalizi maalum. Miaka hii ya mwanzo ya mtoto ni muhimu sana kwa ukuaji

wa binadamu!

SCENE FOUR: NIGHT OUTSIDE MR. KASU’S COMPOUND

105. SFX: WIND BLOWS HARD AND THUNDER

106. SFX: TWO PERSONS RUN FAST ON A GRAVEL ROAD

107. **Challa:** **(Still running fast)** Yarabi! Huyo bwana amempiga risasi Jonas, Siyo?

108. **Mekete:** **(Out of breath)** Ndiyo! Alimpiga risasi! Lakini mbona huyo bwana alianza kupiga kelele BAADA ya kumpiga risasi Jonas?

109. **Challa:** Sijui. Aah! Siwezi tena kukimbia **(breaths hardly)**. Tusimame hapa. Kuna giza hakuna mtu awezaye kutuona.

110. **Mekete:** **(Stops)** Huyo bwana ni mpumbavu sana!

111. **Challa:** Naam, mpumbavu kweli! Mbona hakupiga risasi hewani kwanza?

112. **Mekete:** **(Shocked)** Challa, ebu tazama pale! Yule si mbwa wako?

113. **Challa:** Achana naye!

114. **Mekte:** Mbwa wako Bobbie amekufa, pia!

115. **Challa:** Hanishughulishi katu! Lau hakula nyama ya

sumu, rafiki yetu asingepigwa risasi! (**between sobs**)

116. SFX: GUN IS BEING RACKED

117. SFX: POLICE'S WALKIE TALKIE FEEDBACK SOUND

118. **Polisi:** Polisi! Msiinue miguu hapo mlipo! Mikono kichwani kisha mlale kifudifudi! Hakuna kupinduka!

119. **Mekete:** (**In a low voice**) Ooh! Mkosi gani huu!

120. **Challa:** (**In a low voice**) Yarabi!

121. **Polisi:** (**Talks in walkie talkie**) Ndiyo! Nimewapata wote wawili!

122. SFX: POLICE'S WALKIE TALKIE FEEDBACK SOUND

OUTRO:

Na hapa tunafikia mwisho wa sehemu ya tisa. Vijana wawili wametiwa nguvuni lakini vipi kuhusu rafiki yao Jonas? Yu hai au ameshafariki? Kwa habari kamili usikose kutegea sikio sehemu ijayo ambayo ndiyo ya mwisho. Kumbuka, ukitaka kuisikiliza hii sehemu tena, au kuwasilisha maoni na mapendekezo, fungua ukurasa wetu wa tovuti to dw.de/lbe. Usikose kujiunga nasi kwenye sehemu ijayo- Kwaheri!